JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

Menejimenti ya
Utumishi wa Umma,
S.L.P. 2483,
DAR ES SALAAM.

Kumb. Na. EA 45/257/01/2

30 Desemba, 2008

# WARAKA WA WATUMISHI NA. 5 WA MWAKA 2008 USAFIRISHAJI WA MIZIGO (PERSONAL EFFECTS) YA WATUMISHI

**Utangulizi:**

1. Utaratibu wa kusafirisha mizigo ya watumishi wanaposafiri kwa ajili ya kuanza kazi, kuhamishwa au kustaafu kazi umefafanuliwa katika Kanuni J4, 8, 9 na 10 za Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la II la mwaka 1994. Kanuni hizi ziliweka viwango vya uzito wa mizigo ya watumishi wanaposafiri katika mazingira hayo kwa kutegemea ngazi zao za mishahara. Aidha, Kanuni hizo zinaelekeza njia za kutumia katika kusafirisha mizigo ya watumishi. Hata hivyo, mbali na kuainisha uzito wa mizigo, Kanuni hizo hazikutaja gharama zinazostahili kusafirisha mizigo hiyo. Hali hii imesababisha matatizo mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Waajiri wamekuwa wakitumia njia tofauti kugharamia usafirishaji wa mizigo ya watumishi;

(ii) Wakati mwingine waajiri wameshindwa kutenga fedha za kutosha katika bajeti zao kwa ajili ya kusafirisha mizigo ya watumishi kwa kuwa hakuna kiwango maalumu kilichowekwa rasmi na Serikali;

(iii) Watumishi wa Umma wanaohitaji kusafirishiwa mizigo yao na Serikali wamekuwa wakipata huduma tofauti kwa kuwa mfumo wa usimamizi hutofautiana baina ya waajiri;

(iv) Matokeo ya jumla yamekuwa yakisababisha usumbufu kwa watumishi wanaposafiri kuanza kazi, kuhama au kustaafu kazi.

2. Kutokana na kasoro zilizoelezwa hapa juu, Serikali imeamua kutoa mwongozo utakaowawezesha waajiri kuwahudumia watumishi wao wanaposafiri katika mazingira yaliyoelezwa katika Aya ya 1 ya Waraka huu.

## UTARATIBU WA KUSAFIRISHA MIZIGO YA WATUMISHI

Utaratibu wa kusafirisha mizigo ya watumishi utakuwa kama ifuatavyo:

(i) **Usafirishaji wa mizigo ya Watumishi:**

Gharama za kusafirisha mizigo ya watumishi wanaposafiri kwa ajili ya kuripoti katika vituo vyao vya kazi wakati wa kuajiriwa mara ya kwanza, uhamisho na kustaafu kazi zitaendelea kutolewa na Serikali.

(ii) **Uzito wa mizigo itakayogharamiwa na Serikali:**

Kiwango cha mizigo ya mtumishi itakayogharamiwa na Serikali kitabaki kama kilivyofafanuliwa katika Jedwali la I (APPENDIX J/I) la Sehemu J ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la pili la mwaka 1994.

(iii) **Aina ya Mizigo itakayogharamiwa na Serikali:**

Aina ya mizigo itakayogharamiwa na Serikali itaendelea kuwa; vifaa vya nyumbani kama vile samani, matandiko na vifaa vya kupikia. **Serikali haitagharamia** vifaa vingine vinavyoweza kutumika kama biashara, kwa mfano mbao, mabati, sementi, mifugo, mazao mengi ya shambani, gari au mashine.



(iv) **Gharama za kusafirisha mizigo:**

Serikali itagharimia usafirishaji wa mizigo kwa kiwango cha shilingi 1,000/= kwa tani moja kwa kilomita. Serikali itakuwa ikihuisha viwango hivi mara kwa mara kulingana na soko la usafirishaji mizigo nchini baada ya kushauriana na vyombo au Taasisi husika.

**Utekelezaji:**

4. Katika kuhakikisha utekelezaji wa maamuzi haya ya Serikali, kila Afisa Masuuli atatakiwa kutenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya kugharamia usafirishaji wa mizigo. Pale ambapo Maafisa Masuuli watahitaji kujiridhisha na umbali baina ya vituo wanavyotoka na kwenda watumishi wanaohitaji kusafirishiwa mizigo. Idara zinazohusika na ujenzi wa barabara au Wakala wa barabara (TANROADS) zilizoko karibu zishirikishwe ili kubaini umbali baina ya vituo hivyo.

**Tarehe ya kuanzia kutumika:**

5. Waraka huu utaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2009 na utasomwa kwa pamoja na sehemu "J" ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la II (1994).

GEORGE D. YAMBESI,
*Katibu Mkuu (Utumishi)*